

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

[JUE SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI]

VITENDO VINAVYOKATAZWA NA SHERIA  
YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

### Wasiliana nasi

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa  
Viwanja vya Nanenane Nzuguni  
Jengo la Wizara ya Kazi - Mtaa wa Nzuguni A  
S.L.P 2851  
**DODOMA**

## *Sehemu ya tano(5) ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi*

Sheria ya Gharama za Uchaguzi inakataza vitendo vifuatavyo kabla na wakati wa mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa kwa mtu aliyetangaza au kufanya vitendo vinavyoonesha nia ya kushiriki katika mchakato wa uteuzi, wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa, kampeni za uchaguzi na uchaguzi:

- i) Kutoa fedha, mikopo au kitu chochote chenye thamani ili kumshawishi mtu kupiga au kutopiga kura (Kifungu 21(1)(a)).
- ii) Kuahidi au kutoa ajira, wadhifa sehemu ya kazi ili kumshawishi mtu kupiga au kutopiga kura (Kifungu 21(1)(b)).
- iii) Kutoa zawadi, mkopo, msaada, ahadi, kununua kitu chochote au kuingia makubaliano na mtu mwingine, ili kupata uteuzi (Kifungu 21(1)(c)).
- iv) Kutoa au kuwezesha kupatikana kwa uteuzi kutokana na zawadi, mkopo, msaada, ahadi au makubaliano yaliyoingiwa baina ya wahusika (Kifungu 21(1)(d)).
- v) Kulipa au kuwezesha kulipwa fedha ili zitumiwe kwa ajili ya hongo (Kifungu 21(1)(e)).
- vi) Kupokea au kukubali kupokea fedha, zawadi, mkopo, msaada, ahadi, wadhifa au kitu chochote chenye thamani ili upige au usipige kura. (Kifungu 21(1)(f)).
- vii) Kupokea fedha au kitu cha thamani kutoka kwa mtu aliyepiga au ambaye hakupiga kura, baada ya kumshawishi kupiga au kutopiga kura (Kifungu 21(1)(g)).
- viii) Kutoa, kulipia au kupokea chakula, vinywaji, burudani kwa njia ya rushwa ili kumshawishi mtu kupiga kura au kutopiga kura (Kifungu 22 (a) na (b)).
- ix) Kulipa au kuingia mkataba wa kulipia kusafirisha wapiga kura (Kifungu 23(1)(a), (3), (4) na (5)).
- x) Kutumia nyumba, ardhi, jengo au eneo lolote kinyume cha sheria (Kifungu 23(1)(b)).